**UKAGUZI WA VITABU VYA MAMBO YA NYAKATI -ESTA** (Eddy Gilpin)

Vitabu vilivyotajwa,Mambo ya Nyakati wa Kwanza na wapili kiasili vilikuwa ni kitabu kimoja. Vilionekana hivyo na Wayahudi ( kama ilivyo vitabu vya Samweli,Wafalme pamoja na vingine). Hivi viligawanywa kama vitabu viwili tofautu wakati wa Septugenti ilipofanyika. ( utafsiri wa Kiyunani wa Lugha ya Kiebrania wa Agano la Kale).Mambo ya Nyakati wa kwanza na wapili ni vitabu vilivyovuviwa (Kupewa pumzi ya Mungu). Chaguo la mwandishi wa vitabu hivi kama ilivyo kwa wasomi waliowengi na tamaduni za Wayahudi ni Ezra (hata kama vitabu vyenyewe havimfunui kama ni muandishi).Vitabu hivi vinaweza kudondolewa kama ifuatavyo:-

1. Vizazi (1 Nyakati 1-9)
2. Utawala wa Daudi (I Nyakati 10-29)
3. Utawala wa Solomoni (II Nyakati 1-9 )
4. Historia ya Wafalme wa Yuda (II Nyakati 10-36)

Imependekezwa kwamba vitabu viwili vya Nyakatii viliandikwa kwa wale waliorudi toka utumwani Babeli (kama ilivyo kinyume na vitabu viwili vya Wafaleme viliandikwa hasa zaidi kwa wale waliokuwa utumwani Babeli).Ukifuatilia orodha ya vizazi katika sura ya kwanza hadi ya tisa, na kuanza kwa Utawala wa Daudi,Sura ya kumi ya kitabu cha Mambo ya Nyakati wa kwanza kinafunua siku za mwisho za Mfalme Sauli-vita alivyopigana na Wafilisti, kifo cha watoto wake,na kujinyonga kwake na kuzarauliwa kwa mwili wake na Wafilisti. Sura zilizobaki zinashulighulikia mambo mbalimbali ya maisha ya Daudi. Ikiwa ni pamoja na kuchaguliwa kwake kama Mfalme (na pia Yerusalemu kama mji mkuu); maelezo ya Uzzia na sanduku la Agano; Daudi akiwashinda Wafilisti ( na mataifa mengine yaliyo maadui kwa Waisraeli); kulirudisha sanduku la agano nyumbani;ahadi kwa Daudi kwamba mwanae atamjengea Mungu nyumba (kama sehemu ya unabii kuhusu Kristo); Daudi akiwahesabu Waisraeli na adhabu iliyofuata; kuanzishwa kwa ukuhani: Daudi akiandaa vitu vya kujengea hekalu;kupakwa mafuta kwa Sulemeni kama Mfalme; na kifo cha Daudi.Mambo ya Nyakati wa pili inaanzia na mwishilizio wa Mambo ya Nyakati wa Kwanza . Inaanza na na Sulemani kutamani kuwa na hekima toka kwa Mungu, maombi ambayo alipewa. Na zaidi inaeleza sulemani anvyojenga hekalu na vyote vilivyohusika nalo, na pia kulitoa na kutokewa kwa utukufu wa Mungu juu yake. Maagizo ya ahadi ya Mungu kwa Sulemani yanatolewa kwa undani. Miji iliyojengwa au kurejezwa na Sulemani nyumbuliwa. Utukufu wa Sulemani dhidi ya Ufalme unafunuliwa na mambo kama kutembelewa na Malkia wa Sheba na maelezo bahati aliyoipata.Wakati wa kifo cha mwanae, Rehoboamu afanyika kuwa Mfalme.

Sehemu ya Mwisho ya Waamuzi wa pili (Sura ya 10-36) inaonyesha mgawanyiko wa Ufalme na inatuambia hasa kutengana kwa Wafalme wa Ufalme wa kusini (Yuda). Wafalme wa kaskazini (Israeli) wametajwa tu kwa muda na wakati na kwa namna walivyohusika na Ufalme wa Yuda na Wafalme wake. Kwa hakika, Wafalme wote wa Yuda wametajwa katika kipengele hiki; lakini kati yao jumla ya kumi na tisa ni Wafalme wa Israeli, watano pekee wametajwa kwa majina (Yeroboamu;Bashaa;Ahabu;Ahaziah;na Yoashi). Kipengele hiki kinahusika mgawanyiko wa ufalme na kutengwa kwa baadhi ya wafalme wakuu wa Kusini (Rehoboamul Asa; Yehoshafati; Ahazia; Athalia;Uzzia;Hezekia;Manasse; na Yosia). Karibu kabisa na Mwisho wa kitabu cha Mambo ya Nyakati wa pili hali ya masikitiko ya Yuda inaelezwa kwa maneno haya:

"Na zaidi ya hayo wakuu wote wa makuhani , na watu, wakakosa mno sawasawa na machukizo yoye ya mataifa , wakainajisi nyumba ya BWANA, aliyoitakasa katika Yerusalemu. Naye BWANA, Mungu wa baba zao,akatuma kwao kwa mkono wa wajumbe wake, akiondoka mapema, na kutuma; kwa sababu aliwahurumia watu wake, na makao yake; lakini waliwadhihaki wajumbe wa Mungu, na kuyadharau

maneno yake, na kuwacheka manabii wake, hata ilipozidi ghadhabu ya BWANA juu ya watu wake, hata kusiwe kuponya."(II Mambo ya Nyakat 36:14-16).

Hata hivyo, kitabu kinamalizia (miaka sabini baadaye) na mistari miwili inazungumzia koreshi, Mfalme wa uajemi aliyewaruhusu watu wa Yuda kurudi katika nchi yao.

Sehemu ya kitabu cha Ezra na Nehemia zinalingana ( kama kitabu cha Hagai na Zakaria); pia kitabu cha Esta kinaweza kuwekwa katika mlolongo wa kipindi cha Ezra.Kitabu cha Ezra kinahusu mambo ya wakati mara tu ya mwisho wa utumwa wa Babeli. Hakika, mistari mitatu ya mwanzo ya Ezra ni karibu neno kwa neno na mistari miwili ya mwisho ya Mambo ya nyakati wa pili. Kitabu cha Ezra kinahusisha majaribio na mafanikio ya mwisho ya kurudi toka utumwaani Babeli (Wakiongozwa na Zerubabeli) katika harakati zao za kulijenga tena Hekalu (Sura ya 1-6).Baada ya miaka sabini, hatimaye kazi likamilika (Ezra 6:15). Ni takribani kama miaka 57 kipindi cha kuunganisha kati ya Ezra 6 na Ezra 7 ambapo kitabu cha Esta kinakamilisha mfululizo.Sura zinazobaki za kitabu cha Ezra (7-10) zinaonyesha kurudi kwa Ezra na wengine (kwa waraka wa Ataxerxers),Juhudi zake kurejeza kanuni na sheria za Musa kwa watu ambao wamerudi utumwani na kuwasihi ni vema kuzitunza, na anavyoshughulika na mambo magumu ya kuoleana kwa baadhi ya Wayahudi na watu wa kipagani wa nchi ile.

Kitabu cha Nehemia kinashughulika na ujenzi wa ukuta kuzunguka Yerusalemu(Sura ya 1-7), kuwasomea sheria na kuwasihi juu ya uaminifu kwayo (Sura ya 8-12), Nehemia akishughulikia matatizo mbalimbali ambayo yalijitokeza(Sura ya 13). Kujenga upya ukuta kulikuwa kugumu sana kwa sababu ya maadui (Sanbalati, Tobia,na Gesheni). Hata hivyo juhudi zao za kuwazuia kumaliza kazi haikufanikiwa (Nehemia 6:15).Kufuatia kumalizika kwa kazi ya kujenga ukuta, watu walisimama na kusomewa sheria, na waliagizwa na Ezra, Nehemia na Walawi kuhusu wajibu wao kwa Mungu. Wafundishwa pia baadhi ya mambo kuhusu historia na urithi wao.Kitabu kinamalizia na Nehemia akishughulikia mikataba na Eliashibu, kuwarudishia Walawi sehemu yao,kusimama kwake imara juu ya kushika siku ya sabato, na tatizo la kuingiliana katika ndoa na wageni.

Kitabu cha Esta ni cha kufurahisha zaidi! Kinashughulika na kipindi cha utambulisho wa historia ya waisraeli wakati wa uzao wa Abrahamu ulipodhihakiwa, pamoja na ahadi zilizoambatana na uzao wake (Kristo) ambaye ataubariki ulimwengu. Hata ingawa jina la Yehova halitajwi katika kitabu hiki, Mkono wake unaotoa bado unatenda kazi, ukihakikisha kwamba kilichozarauliwa hakitapita.Wenyeji walianza kuwakataa na tena Malkia Vashti kukiuka kanunu zake za utawala mbele ya mumewe aliyelewa. Wakati alipopata fahamu, kutafuta kurudisha kulimrejesha mwanamke myahudi Binamu yake mkubwa na Esta,Modekai, ambaye alikuwa mlinzi wake wakati wote huo, na aliendelea kuwasiliana naye. Kama maelezo yanavyo mzungumzia mtu huyu Hamani aliyepata cheo kikubwa katika himaya ya Mfalme. Kwasababu ya kumchkia Modekai, Hamani alimuahidi Mfalme kwa kutoa tamko kwamba wayahud wote wauwawe kwa siku iliyoichagua. Mfalme bila ya kutambua kwamba Malkia ni wa ukoo ule, alitia sahihi maombi ya Hamani. Modekai aliposikia jambo hilo na kumsihi Esta ili kumsihi Mfalme juu ya watu wake. Hata hivyo alikuwa akisita kufanya hivyo (Kwa sababu kwenda kwa Mfalme bila mwaliko inaweza kukusababishia kifo), aliwenda kwa Mfalme na alikubaliwa kuonana naye. Ombi lake lilihusisha kula chakula la Mfalme pamoja na Hamani, ambapo ombi lake likapokelewa.Wakati wa chakula aliweka wazi na kujitambulisha kuwa yeye ni Myahudi na shauri la uongo la Hamani kutaka watu wake wauwawe. Kwa hasira, Mfalme aliondoka mle kwenye chumba, na kurudi na kumkuta Hamani akiwa amelala katika kitanda cha Esta,akimsihi juu ya maisha yake. Kwa ukali Mfalme alitaka Hamani anyongwe juu ya yale yale aliyomuandalia Modekai. Na, ingawa Mfalme hakuweza *Kulipa* shauri la uovu la Hamani, alitoa shauri jingine ambalo liliwaruhusu Wayahudi kujilinda na kupigana dhidi ya wale watakaotaka kuwauawa. Mwisho, Wayahudi waliachwa, uzao wa Abrahamu uliendelea, na Modekai ali inuliwa kuwa mtu wa pili katika Ufalme wake Ahasuero.